

# ARDHI, MABADILIKO YA TABIA NCHI, NA JINSIA

care

HAKIARDHI
LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

Tanzania Natural Resource Forum
Jumuiko la Maliasili Tanzania

## UTANGULIZI:

Ardhi Yetu (AYP +) ni programu ya kitaifa inayohusika na utetezi wa haki za ardhi kwa kuimarisha utekelezaji wa shughuli ndani ya jamii huku ikijenga uwezo wa kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

AYP+ imjejikita katika kujenga uwezo wa asasi za kiraia nchini, kuimarisha makongamano ya kitaifa, na majukwa ya pamoja ya utetezi yaliyoanzishwa wakati wa awamu ya kwanza ya Programu hii.

Dhumuni la programu ni kufanikisha lengo lake kuu la kuwa na jamii na asasi za kijamii zinazofanya utetezi juu ya kuwepo kwa sekta ya ardhi jumuishi na wazi, haki ya umiliki wa ardhi iliyoimarishwa, jamii za wafugaji na wakulima wadogo wenye uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi —hususani wanawake.

Mradi huu unashirikiana na wabia mkakati watatu: Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF), Taasisi ya HAKIARDHI , na Asasi ya kiraia inayofanya kazi na jamii za kifugaji PAICODEO.

Mradi unafadhiliwa na shirika la CARE Denmark kupitia CARE nchini Tanzania. Mradi unafanya kazi katika wilaya 10 ambazo ni Iringa vijijini, Chemba, Kiteto, Simanjiro, Kilolo, Mufindi, Morogoro, Kilombero, Mvomero na Kilosa.

Programu hii inaendana na dira inayotaka kuona jamii yenye nguvu na sauti ambazo ni chanzo cha suluhu za uhakika za umiliki wa ardhi na uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Uwezo wa uhimilivu ni suala nyeti na jipya ambalo lilianzishwa kwa kutambua kuwa uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi utategemea usimamizi endelevu wa ardhi na maliasili.
Malengo mahususi ya AYP+ ni:

**Jamii:** Jamii inauwezo wa kusimamia na kudhibiti visababishi vya hali hatarishi (Mabadiliko ya tabianchi, usimamizi wa maliasili, upatikanaji wa ardhi, masuala ya usawa wa jinsia), na serikali za vijiji/mtaa zinazowajibika kwa jamii husika.

**Asasi za Kiraia:** Mitandao imara ya asasi za kiraia yenye mawazo yenye mlengo na uwezo wa kufanya kazi kwa pamoja na serikali, sekta binafsi na kuandaa majukwaa yanayotumika kukumbusha wajibu wa serikali na sekta zingine kuhusu sera na programu za ardhi zilizo makini, zenye kuleta uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi, na zenye kuleta uhimilivu, na zilizo jumuishi.

**Serikali/Sekta Binafsi:** Serikali yenye uwazi na usikivu (katika ngazi ya kijiji/mtaa hadi taifa) na ambayo inashirikisha wakulima wadogo na wafugaji katika midahalo inayohusu makabiliano na mabadiliko ya tabianchi.

Programu ya AYP+ inatilia mkazo suala la nafasi ya jamii, jambo ambalo ni muhimu katika kuhakikisha kuwa kampeni na sera za kitaifa na midahalo ya kisera inayoongozwa na wanajami, inajengwa katika misingi na sauti ya jamii, utendaji na hali zao halisi.

Aidha, programu inachukua fursa hiyo kuimarisha usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wa wanawake kwa kujumuisha shughuli mahususi zenye kuleta mageuzi katika suala la usawa kwa namna endelevu na kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030.



## USULI/UTANGULIZI

Zaidi ya asilimia 75 ya watanzania wanaishi vijijini na wengi wao wanategemea kilimo na ufugaji kama chanzo cha kujinasua kiuchumi na kimaendeleo kwa ujumla wake.

Kilimo kimeendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania kikichangia asilimia 25 katika pato la taifa nakuzalisha asilimia 80% ya shughuli za kujikimu. Zaidi ya asilimia 90 ya wanawake wanaojihusisha na shughuli za uchumi hujihusisha na kilimo na huzalisha asilimia 70 ya mahitaji ya chakula.

Kwa mujibu wa takwimu za serikali, wafugaji pia wana nafasi muhimu katika uchumi wa nchi, wafugaji na wakulima wanazalisha asilimia 98 ya ng'ombe 21 milioni na wanyama wadogo 22 milioni, na kuzalisha kiasi kikubwa cha maziwa na nyama nchini (URT 2011).

Kwa wafugaji na wakulima wadogo, ardhi ni tegemeo lao kubwa katika kujipatia uzalishaji endelevu wa shughuli zao

***Wanawake wengi hususan wale wanaoishi vijijini hawana haki ya kurithi, kupata, kumiliki au kutoa maamuzi kuhusu ardhi au mazao yaliyozalishwa juu yake, suala hili linaathiri maisha yao ya kiuchumi na ya kijamii.***

za kujikimu. Licha ya uchangiaji wao mkubwa katika uchumi na uhakika wa chakula nchini, wafugaji na wakulima wadogo, na hususan wanawake, mara nyingi huachwa nyuma katika michakato ya utoaji wa maamuzi yanayohusu ardhi na hivyo kupelekea kupunguza uwezo wao wa kujenga shughuli za kujikimu zilizo endelevu.

Wanawake wengi hususan wale wanaoishi vijijini hawana haki ya kurithi, kupata, kumiliki au kutoa maamuzi kuhusu ardhi au mazao yaliyozalishwa juu yake, suala hili linaathiri maisha yao ya kiuchumi na ya kijamii. Desturi kama hizi huchangia kuwafanya wanawake kuwa maskini.

Hii hukwamisha uwezo wa uzalishaji nchini kutokana na kwamba chini ya asilimia hamsini ya idadi ya watu wote nchini ndiyo inayoshiriki katika shughuli za maendeleo. Tafiti zinaonesha kwamba, upatikanaji na usimamizi wa rasilimali za uzalishaji mali, ikiwemo ardhi, kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake na jamii masikini itasaidia kuwa na uhakika wa chakula na kiuchumi kwa ujumla.

Nchini Tanzania, ardhi imegawanywa katika makundi matatu kwa mujibu wa sheria. Ardhi ya kijiji (70%), hifadhi (28%), na jumla (2%). Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kwamba viwango hivi vya asilimia vinaweza vikawa tofauti na hali halisi.

Ardhi ya kijiji ndiyo inayobeba asilimia 80 ya shughuli za kujikimu za watu; na hii inamilikiwa chini ya mifumo ya kimila ya kumiliki ardhi hivyo umiliki wa kimila ni muhimu sana.



Safari yetu: Kujifunza kutoka kwa wanajamii

Katika kipindi cha zaidi ya miaka mitano, Programu ya Ardhi Yetu kwa kushirikiana na washirika wake (HAKIARDHI, Tanzania Natural Resources Forum (TNRF), AND PAICODEO) imekuwa ikishirikiana na jamii katika kufanya utetezi wa haki za ardhi, usawa wa jinsia, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Lengo kuu la mradi ni kuhakikisha kuwa utetezi wa kitaifa, midahalo ya kisera, na kampeni, zinaongozwa na sauti za wanajamii pamoja na utendaji na hali zao halisi. Ripoti hii inaainisha juhudi binafsi na za pamoja za wanufaika wa mradi,. hususan wanawake.

Uzoefu na sauti zao ni muhimu katika kuongoza shughuli za mradi ili zifikie malengo kwa kuzingatia mitazamo ya jamii ili kufanikisha mabadiliko halisi. Ripoti hii vilevile itatoa maelezo kuhusu programu na washirika wake, namna ambavyo jamii (kwa kupitia juhudi binafsi au kwa pamoja) inashughulikia migogoro ya ardhi, masuala ya kijinsia hususan ukatili wa kijinsia, na/au kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Itasaidia kuelewa zaidi tofauti za kitamaduni na mitazamo kuhusu umiliki wa ardhi, michakato ya utoaji wa hati miliki na masuala ya kijinsia yanayohusiana na umiliki wa mali. Aidha, ripoti inabainisha mafanikio ya wanawake katika kupunguza ukatili wa kijinsia, kuondoshwa katika makazi, na uhaba wa maji. Simulizi za wanajamii zinaonesha umuhimu wa maarifa na uzoefu wa jamii katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

AYP+ na washirika wake inapenda kutambua sauti za jamii, uzoefu, na utayari wao wakueleza uzoefu wa maisha yao ili kuupa mradi changamoto ya kujikita zaidi katika kutafuta suluhu zinazoakisi uhalisia wa maisha ya wananchi.

Haki za Ardhi

Migogoro ya ardhi imekuwa ikiongezeka katika miaka ya hivi karibuni nchini Tanzania. Uhaba wa ardhi na ushindani unaotokana na vipaumbele mbalimbali juu ya matumizi ya rasilimali ardhi imechangia katika kuongeza hali hii. Pamoja na kwamba serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imeandaa mbinu za kukabiliana na changamoto zinazohusiana na ardhi, nyingi kati yao bado hazijapatiwa suluhu.

Tafiti kadhaa zimeonesha kuwa wakati eneo la ardhi ya kijiji linapungua, eneo la ardhi ya jumla na ya hifadhi linaongezeka. Mabadiliko haya huchochea migogoro baina ya watumiaji. Migogoro ni kati ya vikwazo vikubwa vinayokabili haki za ardhi kwa wazilishaji wadogo na hususan wanawake. Mara nyingi migogoro hii hutokea baina ya mtu mmoja mmoja, kijiji kwa kijiji, wanakijiji na mwekezaji, na katika maeneo ya hifadhi, migogoro huwa ni baina ya kijiji na serikali, au hifadhi za taifa na misitu.

Moja ya lengo la AYP ni kufanya kazi na wadau mbalimbali kwa dhumuni la kushughulikia migogoro ya ardhi na kupata suluhu ya kudumu kwa kuwashirikisha wanajamii na watoa maamuzi. Programu ya AYP+ imeweka kumbukumbu ya maandishi kuhusu migogoro iliyopo pamoja na mbinu za ufumbuzi zilizobuniwa na wanajamii baada ya kuwezeshwa na washirika mbalimbali ikiwemo serikali na vitengo vyake katika kushughulikia migogoro hiyo. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya matukio na shuhuda mbalimbali inayoonesha sauti za jamii na uzoefu wake katika kukabiliana na migogoro ya ardhi na namna gani wanatatua.

Migogoro ya Ardhi na Utatuzi

Uondolewaji katika makazi: Athari zake kwa wanajamii hususan wanawake, wazee, na watoto

Moja ya matokeo ya migogoro ya ardhi, hasa kwa makundi yaliyopo pembezoni, ni kuondoshwa katika makazi wanayoishi. Mtindo wa maisha ya kuweka makazi ya kudumu kwa muda maalum ambayo wafugaji wamekuwa wakigeukia katika miaka ya hivi karibuni, umepelekea kuwapo na ulazima wa kuwa na makazi ya kudumu ya moja kwa moja ambamo wanawake wanaweza kulea watoto wao na kuwapeleka shule huku wanaume wakihamahama waktafuta malisho kwa ajili ya mifugo.

Mara nyingi tukisikia kuhusu watu kuondoshwa katika makazi yao, hasa wafugaji mawazo ya wengi hasa wale wasio na uzoefu na wafugaji au namna wafugaji wanavyoishi taswira waliyonayo zaidi ni ile ya mifugo mingi na kundi dogo la watu likihamishwa kupisha hifadhi, au shughuli nyingine za maendeleo.

Kwa watu wengi, ukizungumzia wafugaji, wanawaza kuwa hao ni watu ambao hawakai katika eneo moja, watu ambao hawafahamu nini maana ya kuwa na makazi na ambao wana tafsiri tofauti kuhusu familia.

Hata hivyo, ukifanya kazi na wafugaji utakuta kuwa moja kati ya ndoto zao kubwa ni pamoja na kuwa na sehemu ambayo wanaweza kufanya makazi yao na kupaita nyumbani, mahali ambapo wanaweza kulea watoto wao na kuwapeleka shule, na kupata huduma nyingine muhimu kama afya. Kama jamii ya kifugaji bado wanataka kuhama na mifugo yao ili kupata malisho lakini wakati huohuo waendelee kuwa na sehemu ambayo itakua ni makazi ya nyumbani.

Kuondoshwa kwa watu katika makazi yao kunaathiri zaidi wanawake, watoto na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu.
Hali kadhalika kwa wanawake wajawazito na wale wanaonyonyesha, wazee na wagonjwa. Kwa kufanya kazi na jamii za wafugaji na kusikiliza simulizi kutoka kwa wanawake, wanaume, na kupata undani wa uzoefu wao kulisaidia programu na



Sura za huzuni baada ya kunyang'anywa maeneo yao

washirika wake kuelewa kuwa athari za kuondoshwa katika makazi haziishii katika mali au mifugo pekee.

Inahusu wanawake wajawazito ambao wanalazimika kutembea umbali mrefu,kulala misituni huku wakitafuta makazi mapya, wanawake wenye watoto wadogo, wazee ambao miguu yao haina nguvu ya kutembea, wanawake walioko katika vipindi vyao vya hedhi bila kuwa na nyenzo stahiki,wagonjwa, familia ambazo zinaishia kulala chini ya mti kwa miezi kadhaa huku wakiangalia ni wapi watajihifadhi kesho kwa muda kabla ya kuondoshwa tena.

Watoto wa familia zilizoondoshwa zinajikuta katika hatari ya kupatwa na magonjwa kutokana na baridi, mbu, na kulala kwenye mazingira hatarishi huku kukiwa hakuna huduma za msingi kama vile shule na vituo vya afya. Ni jambo la kawaida kwa familia hasa za kifugaji kulazimika kuhonga viongozi wala rushwa ili waongezewe muda na/au kuepuka kuondoshwa katika maeneo yao. Hii imesababisha kuwepo kwa hofu na hali ya wasi wasi kwa wanajamii ambao mara nyingi hukimbia kila mara wanapoona gari wakidhania ni wale wanaokuja kuwaondosha. Hofu ya kile wasichokifahamu, hali ya wasiwasi na hofu ya kupoteza kile wanachokiita ni makazi yao, ni simulizi zinazosimuliwa sana na wafugaji na wakulima wadogo, hususan wale wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi.

Programu ya AYP na washirika wake walitembelea wanajamii katika kijiji cha Wami Sokoine, Wilaya ya Mvoremo mwezi Agosti 2019, kwa lengo la kujadili masuala yanayohusu ardhi, mabadiliko ya tabianchi na usawa wa jinsia, na kugundua kuwa wanajamii kutoka Ranchi waliondoshwa katika makazi yao tangu Januari 2019. Wanakijiji walieleza kuwa wamekuwa wakiishi hapo kwa zaidi ya miaka 12, na kuwa wanamini kuwa eneo hilo lilitolewa na serikali ya kijiji .

Kwa mujibu wa simulizi ya Bi Amina Msendekwa, kiongozi wa kikundi cha wanawake, “tulipokea barua ya kuwa tutaondoshwa katika makazi yetu, tulienda kumuona Mkuu wa Mkoa ambaye alitupa siku 20 za kujiandaa kuhama katika makazi yetu ingawaje mwanzoni tulipewa siku saba na Mkuu wa Wilaya. Lakini cha kushangaza ni kwamba tuliondoshwa kabla ya siku 20 kumalizika.”

Kama wanajamii hatukupendezwa na namna ambavyo tulihamishwa. Bi Anna Almas anasimulia “tulilazimika kulala chini ya mti kwa hofu kuwa tukibaki kijijini lolote baya linaweza kutukumba sisi na familia zetu.” Kwa wanajamii walioondoshwa wengi wao wamelazimika kuhifadhiwa na ndugu na wengine katika makanisa. Baadhi ya watoto na wazee kutoka katika famiia zilizoondoshwa walipata hifadhi katika nyumba za wachungaji zilizotengwa kwa ajili ya kuwapatia hifadhi. Hata hivyo, nyumba hizo hazikuwa na nafasi ya kutosha na hivyo watoto wengine walilazimika kutafuta hifadhi katika makanisa ya karibu. Hali hii imewaweka watoto na wazee hatarini kupatwa na magonjwa kama vile malaria na nemonia.

***Nyumba yangu pamoja na kila kitu kilichokuwa ndani kiliharibiwa. Nilinunua mijengo 300 na kila moja ilinigarimu shilingi 5,000 kwa ajili ya kujenga nyumba bora. Walikuja wakachoma kila kitu, nyumba yangu pamoja na mijengo niliyoinunua. Nilibaki ni kiwa sina chochote na sitoweza kujenga nyumba nyingine kama hii na sitoweza kununua tena mijengo” alieleza Bi Esther Julius mmoja wa wahanga wa waliondolewa katika kitongoji cha Ranchi kijiji cha Wami Sokoine.***

***“Ndiyo nimemaliza tu kuandaa chakula cha mchana nikaona gari lenu likija. Sikuwaza mara mbili, niliacha chakula changu na kuanza kukimbia nikijua ninyi ni watu wa serikali mliotumwa kuja kutuondosha” Mwanakijiji kutoka kitingoji cha Shamba la Saba.***

Simulizi ya matukio kama haya ya Bi Esther na wengine yamekuwa kitu cha kawaida na hasa kwa wakulima na wafugaji wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi. Uondoshwaji wa watu hufanywa kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupisha miradi ya uwekezaji au kuruhusu uhifadhi wa mimea na wanyama pori,migogoro, ufinyu wa eneo, na nyingine nyingi.

Kwa upande wa wale wanaoondolewa hasa wazalishaji wadogo hawaamini kama sababu hizi ni kweli au za msingi bali zenye nia ya kuwageuza watu wanaotangatanga na wasio na makazi maalum na hivyo kuendelea kuwa masikini.

Simulizi hizi zinadhihirisha kuwa kuna haja ya wataalamu, serikali na wadau wengine kutazama kukaa pamoja na kutafuta muafaka utakaosaidia pande zote kunufaika hasa wazalishaji wadogo bila kuathiri maana kubwa ya kimaendeleo. Kuhamishwa mara kwa mara, na migogogoro isiyoisha ina madhara siyo kwa jamii husika tu bali azima nzima ya Tanzania kutaka kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

# PROGRAMU YA ARDHI YETU+: MBINU ZA UTEKELEZAJI KATIKA KUSHUGHULIKIA HAKI ZA ARDHI, UTATUZI WA MIGOGORO, NA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI KATIKA

Mbinu ya utekelezaji wa programu ni pamoja na kufanyakazi na Waangalizi wa Haki za Ardhi, Majukwaa ya wafugaji na wakulima, Wasaidizi wa Sheria, Vikundi vya wanawake, na majukwaa ya Wadau Mbalimbali katika ngazi ya Wilaya.

Waangalizi wa Haki za Ardhi
Hawa ni watu (wanaume au wanawake), waliochaguliwa na wanajamii kwa njia ya kidemokrasia katika maeneo ambapo mradi unatekelezwa na kupewa mafunzo kuhusu haki za ardhi, usawa wa jinsia, na mabadiliko ya tabianchi ili waweze kusaidia jamii katika nyanja hizi. Waangalizi wa Haki za Ardhi vilevile wanajukumu la kuanzisha na kuratibu majukwaa ya ngazi ya kijiji yatakayojadili masuala ya ardhi na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuwezesha kuwepo kwa midahalo kuhusu masuala ya ardhi vijijini.

Hadi sasa programu imeshaandaa Waangalizi wa Haki za Ardhi wapatao 128 na wameweza kushughulikia kesi 100 zinazohusiana na ardhi tangu mwaka 2015. Catherine Lunyungu ni mmoja wa waangalizi wa Haki za Ardhi kutoka kijiji cha Kimande ambaye amefanikiwa kusaidia wajane 6 kati ya mwaka 2018 na 2019 kutatua masuala yanayohusiana na haki za ardhi; na kwa sasa anaratibu kampeni ya upandaji miti akiwa na lengo la kusaidi kila kaya iweze kupanda angalau miti miwili ifikapo Desemba 2019.

Waangalizi wa Haki za Ardhi walieleza kuhusu mafanikio ya mafunzo yaliyotolewa na washirika. Kwa mfano, Ndugu Augustino Sungura (Mwangalizi wa Haki za Ardhi) alisema “kabla ya mafunzo, sikuthamini masuala ya haki ya za ardhi. Kusema kweli, suala la wanawake kutomiliki ardhi au mali nyingine yeyote ile halikunisumbua, ni suala ambalo sikuwahi kulifikiri kabisa. Halikuwa tatizo kwangu. Baada ya mafunzo nilifahamishwa kuhusu masuala



mengi ambayo nilikua ninayapuuzia siku zote, na nilianza kuelewa kuwa ni jukumu langu kuwaunga mkono watetezi wa haki.”.

Akitoa mfano, Ndugu Sungura aliongeza kuwa; “Mwanahawa ameolewa katika ndoa ya zaidi ya mke mmoja, mume wake alipooa mke wa pili alimtelekeza, akachukua shamba lake na kumwacha na watoto na robo tu ya shamba. Mwanahawa aliposikia kuhusu shirika la Jumuiko la Maliasili na mafunzo kuhusu haki za ardhi, alijiunga mara moja na semina hiyo huku akipigania shamba lake. Kwa kusaidiwa na Waangalizi wa Haki za Ardhi, Uongozi wa Kijiji na Askari Polisi, Mwanahawa alipatiwa kipande kipya cha shamba kwa ajili ya kulima.”

Ndugu Kletus Luvanga, alisema kuwa mafunzo yalimsadia sana yeye na wanajamii wengine, na kuwa kwake mafunzo yamemsaidia sana na sasa anaishi kwa amani na jirani zake pamoja na kaka yake ambaye amekuwa akipambana naye kwa miaka mingi katika mgogoro wa ardhi.

Katika mkutano, baadhi ya washiriki walieleza namna walivyofaidika kwa kupitia mafunzo, na kutaja kuwa kuna mabadiliko makubwa katika masuala yanayohusu ardhi katika kijiji cha Itunundu, hii ni pamoja na kuwa na uwakilishi sawa wa wanawake katika utoaji maamuzi na umiliki wa mali wa hamsini kwa hamsini, kama wengi wanavyoiita. Miaka ya nyuma wanaume wengi wa kijiji cha Itunundu walipinga suala la wanawake kumiliki ardhi kwa kigezo kuwa ardhi ni kitega uchumi chao kikuu.

Hata hivyo, baada ya kushiriki katika mafunzo wanaume wengi sasa wanauelewa mzuri na wapo tayari kumuona mwanamke akimiliki au kurithi ardhi kutoka katika familia zao au waume wao. Wanaume vilevile wamebadili mitazamo yao juu ya wanawake na ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi.

Bi Innochensia Kidunye mmoja wa wanufaika na mradi alisema , “baada ya kifo cha baba yetu, kaka yangu alinikatalia nisimiliki sehemu ya ardhi ambayo alituachia baba, tulikuwa maadui na tulirushiana maneno mabaya sana. Baadaye tulishiriki katika mafunzo ya haki za ardhi, baada ya mafunzo kaka yangu alikubali tuchangie sehemu ya ardhi aliyotuachia baba.

Nilipewa ekari moja na nusu na sasa tunaishi kwa amani.”

Mifano hii inaonesha umuhimu wa suluhu zinazobuniwa na wanajamii katika kukabiliana na changamoto zao. Waangalizi wa Haki za Ardhi ni wawakilishi wa jamii waliochaguliwa ambao wanajiamini baada ya kujengewa uwezo kwa kupitia mafunzo yanayowapa ujuzi na stadi zinazohusu masuala ya kisheria hususan utatuzi wa migogoro ya ardhi, maarifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uwezo wa

kustahimili mabadiliko hayo. Mchango wao ni muhimu katika kuleta mafanikio endelevu ya shabaha na malengo ya programu na kuwezesha jamii kumiliki na kusimamia masuala haya hata baada ya mradi kumalizika.

Majukwaa ya Wakulima na Wafugaji
Majukwaa ya Wakulima na Wafugaji ni majukwaa yaliyoanzishwa kwa lengo la kuwezesha majadiliano kuhusu changamoto mbalimbali zinazokabili jamii na hii ni pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Majukwaa haya yana mchango mkubwa katika kukutanisha pamoja wakulima na wafugaji katika meza moja ya majadiliano ili kushughulikia changamoto zinazowakabili na namna gani wanaweza kumaliza kero zao.

Kwa mfano; mmoja wa wanachama alisema kuwa 'Migogoro katika kijiji chetu cha Itunundu ilikuwa ikitokea mara kwa mara, na wakati mwingine wapo watu waliopoteza maisha. Baada ya miaka mingi ya migogoro, tuliamua kuanzisha jukwaa ambalo litakutanisha pande zote ili tupate suluhu ya kumaliza migogoro na ndiyo maana tumeweza kupata mafanikio. Kwa mfano, mwaka 2016 mmoja wa wakulima (Fidelis Ngalowoka) aliuwawa na wafugaji, hii ilikuwa ni fundisho kwa pande zote mbili, na ilibidi tuchukue hatua na ndipo hapo "jukwaa" lilipozaliwa.

Pande zote mbili ziliamua kufanya majadiliano na kukubaliana kuhusu taratibu watakazofuata katika kutatua migogoro ndani ya jamii zao. Ilipitishwa kuwa wafugaji watachangia katika huduma za jamii kijijini na wao watapewa haki ya kulishia mifugo yao katika mashamba ya wakulima mara baada ya mavuno kufanyika.

Kupitia mpango huu imewezekana kujenga darasa katika shule ya msingi ambapo watoto wa wakulima na wafugaji wote wanatumia kusomea. Mmoja wa wakulima alisema kuwa, 'kabla ya mafunzo, nilikuwa nikiona ng'ombe na wafugaji kama maadui zangu, lakini leo nina mtazamo tofauti'. Akichangia hoja iliyotolewa na wengine, Ndugu Samato (mfugaji) alisema; "baada ya kupata mafunzo na kufanya kazi kwa pamoja chini ya jukuwaa, tulianza kujiona kama wanafamilia na siyo maadui tena.



Kijiji cha Itunundu sasa kina jengo ambalo lilijengwa kwa kupitia michango yetu. Ninavyoongea sasa hivi, lipo jengo la darasa ambalo limekaribia kumalizika". Kuna jumla ya madarasa 5 ambayo yamejengwa kwa michango ya wafugaji. Mwenyekiti wa kijiji cha Itunundu alisema, "watoto wa wafugaji wanaosoma katika shule yetu ni 20 kutoka kwa jamii ya Wamaasai na 50 kutoka kwa jamii ya Wasukuma".

Mapatano baina ya wakulima na wafugaji yalifanyika kati yao bila ya uongozi wa kijiji kuingilia kati. Baada ya kukubaliana kuhusu kiasi cha kuchangia, kamati iliundwa na wanachama kutoka kwa wakulima na wafugaji, iliundwa kwa ajili ya usimamizi wa fedha na mradi wa ujenzi. Kamati itaongoza kwa kipindi cha miaka mitatu tu hadi hapo wanakijiji watakapoamua vinginevyo. Kamati iliyoshikilia uongozi kwa sasa itamaliza muda wake mwaka huu 2019.

Mtunza fedha huchaguliwa na wanajamii ili kusimamia fedha na kuhakikisha kuna matumizi stahiki ya rasilimali. Kiasi cha michango kinategemea eneo la malisho wanalotoa wakulima na kuwapa wafugaji bila kujali kama linamwagiliwa au linategemea mvua. Kwa mfano, michango iliyopitishwa kwa ajili ya kipindi cha 2017-2019 ilikuwa ni kama ifuatavyo:

- 2017 Tsh 6,000,000
- 2018 Tsh 3,000,000
- 2019 Tsh 2,500,000

Kupungua kwa kiasi cha michango iliyokubaliwa inatokana na ukame uliopo katika maeneo husika katika miaka ya nyuma.

Majukwaa ya Wilaya ya Wadau Mbalimbali
Majukwaa ya Wilaya ya wadau mbalimbali ni majukwaa ya majadiliano yaliyoanzishwa katika ngazi ya Wilaya na yana wawakilishi kutoka ngazi ya kijiji, kata, tarafa, na wilaya. Majukwaa ya Wilaya huandaliwa na Asasi za Kiraia na mashirika ya kijamii kwa



kushirikiana na wilaya husika. Majadiliano katika ngazi ya wilaya huandaliwa kwa kupitia vikundi ndani ya jamii, kijiji, kata na wilaya. Majadiliano katika ngazi ya wilaya ni muhimu kutokana na aina na tabia ya wadau wanaoshiriki.

Katika ngazi ya wilaya majadiliano yanaweza kushirikisha sehemu kubwa ya wadau wakiwemo watoa maamuzi, watu wenye ushawishi, pamoja na wanajamii wakishiriki moja kwa moja au kwakupitia wawakilishi wao kutatua changamoto zinazowakabili.

Mchango wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika kuboresha maisha ya wanajamii

Mipango ya Matumizi ya ardhi ikitekelezwa kwa namna shirikishi, ni kati ya nyenzo muhimu inayoweza kupunguza migogoro inayohusiana na ardhi. Inasaidia jamii kufahamu kiasi cha rasilimali ardhi waliyonayo, namna bora ya kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao na zile zinazomilikiwa kwa pamoja na jamii jirani. Ikitekelezwa vyema inarahisisha michakato ya usimamazi na ugawaji wa ardhi kwa watumiaji na watoa maamuzi. Mbali na kupunguza migogoro, mipango ya matumizi ya ardhi vilevile inaweza kuboresha shughuli za kiuchumi na za kujikimu na kuwezesha umiliki wa ardhi kwa wanawake na utoaji maamuzi.

Majadiliano kati ya timu ya Programu ya AYP na wanajamii wa kijiji cha Kilolo ambako mchakato wa Mpango wa matumizi ya ardhi ulifanyika ulipokelewa kwa hisia tofauti kati ya wanaume na wanawake kuhusu uwezo wa mipango hii kuboresha shughuli zao za kujikimu na kiucuhumi.

Wanawake wengi walidhani kuwa mchakato huu unalenga kumwezesha mwanamke kumiliki ardhi chini ya jina lake au kwa pamoja na mwenzi wake. Hii ilikuwa ni muhimu kwao kwani inamwezesha mwanamke kufanya maamuzi kuhusu matumizi ya ardhi na vilevile waliona itampatia mwanamke uhakika wa umiliki iwapo lolote litamfika mume, au mzazi. Ardhi ilitizamwa kama ishara ya kutambulika na kuwa huru hususan katika tamaduni ambako wanawake hawatambuliwi kama wamiliki wa mali bali wakodishaji.

Wanaume nao walithamini mchakato huo kutokana na manufaa yake kwani wanapata uhakika wa umiliki wa ardhi kwa njia ya hati miliki. Kwa mfano, Ndugu Misted (kiongozi wa kimila) alisema, “jambo pekee ambalo tuna uhakika nalo ni hili la haki miliki ya ardhi yetu, sasa tunajua kuwa hakuna atakaye kuja hapa na kutunyang’anya ardhi yetu, kutakuwepo na mazungumzo, lakini kwa upande wa kuboresha maisha bado tunafanya mambo kama tunavyofanya siku zote. Kiwango cha maisha yetu kiko vilevile, zaidi ya kuwa na hati miliki ya pamoja hakuna kilichobadilika”. Aliongeza kuwa wangependa waweze kutumia hati miliki yao ya kimila kupata mikopo kwani kwa sasa haiwasaidii. Suala la mkopo na mali isiyohamishika lilipoingia tulipendekeza tufanye majadiliano kuhusiana na suala hilo na athari inayoweza kuwapata na kama huo ni uamuzi mzuri au kama ni kipaumbele. Lengo lilikuwa ni kufanya kazi na wanajamii, ili waweze kufanya maamuzi sahihi kuhusu ardhi na matumizi yake, kama kigezo cha mali isiyohamashika, na mwishoni wawe na uwezo wa kuamua kuhusu namna ambavyo ardhi yao itatumika.

# Jinsia: usawa na mitizamo mchanganyiko kuhusu dhana ya usawa

Faida ya kumiliki ardhi na mali nyinginezo

Moja ya mambo muhimu yanayojadiliwa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa ni faida ya hati miliki kwa jamii. Ipo mifano na tafiti zinazodai kuwa umiliki wa ardhi hautakiwa kuishia tu katika suala la kuwa na hati miliki katika mfumo wa cheti bali uangalie zaidi namna ambavyo mchakato na hati hiyo inawezesha kuleta maboresho ya kiuchumi na ya kijamii kwa wanajamii husika.

Wanakijiji kwa pamoja wakiongelea juu ya umuhimu wa hati miliki walieleza yafuatayo;

Bi Theresia: "kwanza kabisa kuna uhuru ukiwa unaamua ufanye nini na ardhi yako, unaweza ukawakodishia watu, kujiunga na vikundi vya mikopo, na hata kuitumia kama kigezo cha mali isiyohamishika ili kupata mkopo wa benki."

Bi Maimuna Mtete aliongeza kuwa, "Sasa ninaweza kutunza watoto wangu na familia ya upande wangu bila kuhitaji kumpigia magoti mume wangu au mtu yeyote ili anipe pesa. Ninaweza kulima mwenyewe, kuuza, kupata pesa, na kuamua nifanye nini na pesa zangu. Naweza ata kuamua kujenga nyumba katika kiwanja changu, faida ni nyingi sana".

Uhusiano kati ya umiliki wa Ardhi kwa wanawake na nafasi yao katika kushiriki kufanya maamuzi

"Ata kama nitaamua kununua ardhi yangu mwenyewe, katika mila yetu, mume wangu ananimiliki mimi na mali zangu.

Mimi mwenyewe pamoja na kila kitu ninacho kimiliki kiko chini ya mamlaka ya mume wangu kwa sababu mimi ni sehemu ya mali zake" anasema Bi Hamida Juma kutoka kijiji cha Zambia.


Maelezo ya Bi Hamida yanafanana kwa kiasi kikubwa na hoja za wanawake wengine wengi wanaoishi katika kijiji cha Zambia na kwingineko. Wengi wao wanatambua kuwa suala la kumiliki kwao ardhi ni haki yao na haitakiwi iwe sehemu ya mapatano ya kuolewa.

Hata hivyo wanawake wote wanakubali kuwa umiliki wa ardhi kwa mwanamke ni nyenzo muhimu itakayosaidia kuleta ukombozi wa mwanamke kiuchumi na kijamii kama anavyothibitisha Bi Paulina Lazaro mmoja wa wanawake wenye hati miliki.

"Ninayo furaha kubwa kwani sasa nina ardhi pamoja na hati miliki ya kwangu mwenyewe. Mimi kama mwanamke wa kimaasai hili ni jambo kubwa". (Picha ya Bi Paulina).

Bi Sabina Daniel wa kijiji cha Loonderkes anasema; Ni muhimu kwa mwanamke kuwa na mali yake mwenyewe mbali na zile za pamoja ndani ya ndoa. Wanaume wakati mwingine hawaaminiki hususan pale wanapokuwa hawana pesa kwani wanaweza kuuza chochote.

Mimi na mume wangu tunamiliki shamba



*"INinayo furaha kubwa kwani sasa nina ardhi pamoja na hati miliki yangu mwenyewe. Mimi kama mwanamke wa kimaasai hili ni jambo kubwa".*

la familia na vilevile nina miliki viwanja vingine viwili ambavyo nilipewa na familia ya nyumbani kwetu.

Tamanio langu kubwa ni kupata hati miliki ya viwanja vyangu viwili ili iniwezeshe kuamua ama kukijenga au kukitumia kwa ajili ya malisho ya mifugo. Kuwa na umiliki kunanifanya nijisikie vizuri na nitaweza kutoa ardhi yangu kwa yule mtoto anayenitunza vizuri sasa au baadaye nikiwa nimekwishazeeka.

Ardhi ni kama hazina yangu ya baadae siku za uzeeni. (picha ya Bi Sabina)

"katika mila yetu, mwanamke mwenye watoto ana uwezekano mkubwa wa kurithi mali zaidi ya yule ambaye hana watoto.

Mwanamke mjane na ambaye hana watoto ana hatari ya kuishi bila kuwa na chochote." … "kama watoto wake ni wadogo, ndugu wengine wanaume wataamua juu ya mali alizoachiwa kwa niaba yake kwa sababu ardhi katika kijiji cha Zambia ni mali ya wanaume".

Simulizi za Bi Mariam Omary na Bi Mariam Mandia.

Bi Winfrida Humba
'Huko nyuma katika jamii yetu, wanawake waliishi kama watumwa, hawakuwa na nyumba na hawakuruhusiwa kurithi kwa familia ya baba yao au kwa waume zao.

Tunashukuru kwa kuwa leo hii mambo yanabadilika na wanaume wengi wanaanza kuhamasika kuhusu masuala haya', alisema Bi Winfrida Humba. Akieleza zaidi kuhusu kisa chake alisema:

"Baada ya miaka 27 ya ndoa, mume



wangu sasa anajua kuwa hawezi kufanya maamuzi yeye mwenyewe au kuuza mali zetu zozote zile bila ya mimi kuridhia. Akiamua kuoa tena hiyo ni juu yake, lakini hatochukua mali zetu ili kumpa mke mpya, na hilo analifahamu". Hivyo, kwa kweli masuala haya hayaniumizi kichwa tena."

Ngugu Shaban Kodi akiunga mkono simulizi ya Bi Winfrida anasema; Siku hizi mwanaume hawezi akaamka tu siku moja na kuamua kugawa mali kwa mtu yeyote bila mke kuridhia'. Hatupati kitu tusipo washirikisha wake zetu."

Akiongezea katika mjadala uliokua uanendelea Bi Inochencia John kutoka kijiji cha Itunundu alisema "Kukiwapo na talaka, mwanamke (aliyetalikiwa) atapatiwa nusu ya mali na ataamua nini cha kufanya na mali hizo ikiwa ni pamoja na kuolewa na mwanaume mwingine.

Mwanamke akiwa hana watoto, mali zitagawanywa nusu kulingana na mchango wa mwanamke katika ndoa na mali zilizopatikana wakati wa ndoa."

Mwanamke mwingine akiunga mkono hoja alisimulia kuhusu uzoefu wake kama mjane: "…wakati mwingine ni bora kutalikiwa kuliko kuwa mjane. Ujane ni jehanamu, ni kitu ambacho usingemwombea hata adui yako. Ukiwa mjane moto wake hausemeki. "

*Mtazamo wa Wanaume kuhusu wanawake kumiliki mali*

*Ndugu Hussein Danda: "Kwa mtazamo wangu watoto wa kike wanatunza wazazi wao vizuri zaidi kuliko watoto wa kiume. Ukiwa na wasichana, mimi kama mzazi nina uhakika kuwa ninaye mtu atakaye nitunza vizuri wakati wa shida. Katika familia yangu, kila mmoja ana kipande chake cha ardhi hii ni pamoja na watoto wa kike. Hivyo hata nikifa leo hakuna yeyote katika upande wa familia ya wazazi wangu atakayepata chochote. Nina ekari 4 tu kwa ajili yangu, vingine vyote vinamilikiwa na watoto na mke wangu"*

*Ndugu Shaban Kodi; "mtoto wa kike akipata chochote kutoka kwa mume au kwingineko, sehemu ya kwanza ambako atapeleka mali ni kwa wazazi wake, lakini hali haitofanana kwa mtoto wa kiume. Wawili hawa wanatofautiana.".*

## Utoaji maamuzi, Umiliki wa Ardhi na Ukatili wa Kijinsia

Uzoefu katika jamii unaonesha kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya utoaji maamuzi, umiliki wa mali, na ukatili wa kijinsia.

Kwa mfano wengi wa wanawake tuliowatembelea ambapo wanawake hawakuwa na maamuzi, au hata kuweza kuzungumza mbele ya wanaume, na au hawakumiliki mali, kiwango cha ukatili wa kijinsia ulikuwa uko juu ukilinganisha na kule ambako wanawake wako huru kutoa maoni yao bila uoga, na walikuwa wanashirikishwa katika maamuzi ya umiliki wa mali au walikuwa wanamiliki mali.

Baadhi ya wanawake waliopo katika maeneo ambapo kuna viwango vya juu ya ukatili wa kijinsia hawakua huru kuzungumza kuhusu masuala haya, hii ni wakati wanaume hawapo mbele yao, walibainisha kuwa hali hiyo ilitokana na kunyimwa fursa ya kushiriki katika michakato ya utoaji uamuzi au kutokumiliki mali yoyote ambayo ingeweza kuwapa nguvu au kuwafanya watambulike.

Katika maeneo mengine wanawake walikataa kuongelea masuala haya. Kwa mfano, wanawake wakifugaji (wengi wao) hawakutaka kuzungumzia ukatili wa majumbani ingawaje waligusia kuwa ni jambo ambalo lipo hasa pale waume zao wanaporudi nyumbani wakiwa wamelewa.

Bi Martina Thomas (siyo jina lake halisi) kutoka jamii ya kifugaji alisema, " Ndiyo, ni kweli tunapigwa, lakini haitobadilisha chochote hata tukiongelea kwani hamtokuwepo kusaidia ikitokea, hivyo bora tukae kimwa maisha yaendelee."

Ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake una taswira na vyanzo vingi kulingana na simulizi za wanawake tofauti. Kuna baadhi ya vijiji ambako baadhi ya akina mama waliorodhesha mazingira yanayoweza kusababisha mwanamke kupigwa huku wanawake katika maeneo mengine wakisema hakuna sababu yoyote inayohalalisha mwanamke kupigwa.

Bi Sabrina Timothy (siyo jina lake halisi), ni mama wa watoto saba kutoka Loonderkes alisema, "tunatumia muda mwingi kisimani kutokana na uhaba wa maji unaosababishwa na msimu wa ukame.

Ni jambo la kawaida kabisa kushinda mchana kutwa au usiku mzima kisimani. Tunapochelewa kurudi nyumbani waume zetu hutupiga kwani hawaamini kuwa tulikuwa kisimani muda wote."

Katika kijiji hiki suala la wanaume kupiga wake zao ni jambo la kawaida, wanawake wametafuta mbinu za kujilinda pale panapowezekana.

Kwa mfano, mmoja wa wanawake katika vikundi vya majadiliano alisema; "Ili kujiokoa dhidi ya vipigo vya waume zetu, wanawake waliamua kwamba yeyote atakayepata maji kwanza atasaidia wenzake kupika na kukamua ng'ombe".

Katika mazingira mengine, wanawake waliwaomba waume zao waongee na wanaume wenzao kuwaambia waache kuwapiga wake zao pindi wanapochelewa kutoka kisimani. (picha inahitajika hapa)

Baadhi ya wanawake walisema kuwa

ukatili wa majumbani siyo ubinadamu lakini kutokana na mazingira wanayoishi wanajikuta hawana jinsi ya kuuepuka.

Bi Penina Adam (siyo jina lake halisi), mama wa watoto tisa alisimulia ya kwake huku akiungwa mkono na wanawake wengine;

"tutafanyaje? Tunaishia kulia tu, na kwenda kulala kwenye vyumba vya watoto wetu.

Hatuwezi kuwaacha watoto wetu, hivyo tunalazimika kuendelea kuwepo. Wanaume kijijini kwetu wanaweza kukupiga mahala popote bila uwoga, hata hivyo wao ndio wanaume, wanaweza kutupiga tu. Wanaume wetu wakikasirika hupiga mtu yeyote bila kujali kama ni mke au la. Waume zetu wanaweza kukupiga hata ukiwa ni mjamzito na hawapatwi na lolote."

Bi Mary Fadaina (siyo jina lake halisi) mama wa watoto nane kwa upande wake aliongeza kuwa, "mwanamke akiamua kutoa taarifa, utetezi wake utategemea nani Mwenyekiti wa Kijiji,



kama Mwenyekiti ni mmasai basi jua kwamba hakuna lolote litakaloendelea kwani hata yeye huenda akawa anampiga mke au wake zake, lakini kama Mwenyekiti ni mswahili (siyo mmasai) basi hapo msaada unaweza kupatikana."

Ukatili wa kijinsia hutumiwa na wanaume kama mbinu ya kukandamiza wanawake wasishiriki katika maaumizi. Unazuia sauti ya wanawake na sifa yao ya kuwa chachu pamoja na uwezo wao wa kutoa maamuzi kuhusu umiliki na matumizi ya mali pamoja na mali nyingine za familia.

Bi Patricia Tengayo (siyo jina lake halisi) anasimulia; "nilikuwa nikikodisha ardhi, nikilima na kufanya shughuli zangu zote za shambani, na kuuza mazao, nikipata pesa, mume aananipiga hadi nimpe pesa zote.

Pesa alizitumia kunywa pombe na kwa wanawake wengine. Akirudi nyumbani akiwa amelewa hunipiga tena. Hakuna nililoweza kufanya kwani katika mila za kimasai hakuna talaka.

Baadaye nikajanjaruka na kuanza kuficha baadhi ya pesa.

Sikumwambia tena kuhusu mipango yangu. Bado alinipiga lakini hapati pesa zote. Nina watoto wanne ambao wananitegemea hivyo ilibidi nijifunze namna ya kutafuta maisha. Sijui vipigo vitaishi lini, lakini kwa sasa nina ujasiri wakuficha baadhi ya pesa. (ingiza picha?)

"Katika kitongoji cha Shamba la Saba, "hakuna tofauti kwani mume akikupiga



na ukakimbilia kwa wazazi utapokea kipigo kingine (milanga-fimbo) kutoka kwa wazazi au ndugu wengine hivyo hatuna pakukimbilia."

Bi Lucia Kagangina (siyo jina lake halisi).

Kwa mfano, "mwanaume anaweza kuamua kupata mke mpya bila kumshirikisha mke wake na jukumu la mke ni kuhakikisha kwamba akisikia mume analeta mke mpya anatakiwa akaombe marafiki zake waje wamsadie kuandaa chakula cha mume.

Hatakiwi kuhoji kwani kufanya hivyo kutamsababishia kipigo (Milanga inakuhusu)" Bi Dorothea Tumaini (siyo jina lake halisi)

Hata hivyo ukatili wa kijinsia kama suala lingine lolote lile linalohusu usawa wa jinsia ni changamoto kubwa na lenye mitizamo mbalimbali.

Changamoto hizi hushughulikiwa kwa namna tofauti tofauti, kwa mfano; wanawake katika kitongoji cha Shamba la Saba walisema ukatili huu kama desturi ya jamii ingawaje wanakiri kuwa siyo ubinadamu.

Kwa upande mwingine, wanawake kutoka kijiji cha Lukolongo walionesha mtazamo tofauti juu ya ukatili wa kijinsia.

Hata hivyo, katika baadhi ya vijiji wanawake wanafahamu haki zao na wana uwezekano mdogo wa kukumbana na ukatili wa kijinsia.

Mambo yanayosababisha haya ni pamoja na upatikanaji na umiliki wa ardhi na mali nyingine, utoaji maamuzi katika ngazi ya familia, kuolewa au kutokuolewa, umri na dini.

Vilevile, wanawake katika vijiji hivi wana sauti na wanaweza kudhihirisha mahitaji yao, mambo wanayoyapenda na yale wasiyoyapenda kwa wenzi wao bila hofu.

Bi Happiness Mlongela (siyo jina lake halisi) anasema, "hakuna atakayethubutu kunipiga, mume wangu akifanya hivyo, nitampeleka mahakamani." Mwanamke mwingine aliongeza, mume wangu akijaribu kunipiga, nitamwambia 'hebu nijaribu na utajikuta jela' ataogopa na kuondoka."

Akisimulia uzoefu wake, Bi Alestina (siyo jina lake halisi) anasema “Mume wangu alikuwa akirundi nyumbani akiwa amechelewa na huku amelewa pombe na kunipiga.

Siku moja nikasema sasa imetosha na nikaenda kutoa taarifa polisi, tangu siku hiyo hakujaribu tena ujinga huo.”

Bi Matilda Mtaita (siyo jina lake halisi), mjumbe wa mahakama ya kata alikuwa na simulizi ifutayo;

“Wanawake katika kijiji hiki hawapuzii vitendo vya ukatili wa kijinsia, hivyo tuna wanawake wengi hususan wale wa umri mdogo ambao wanakuja kuomba talaka baada ya kupigwa na waume zao. Ni kwamba hawatovumilia mambo kama haya.

Talaka ni kati ya tatizo kubwa tunalokabiliana nalo, kwa mfano, mwezi Agosti 22, 2019 tuliidhinisha talaka 3. Talaka nyingi zinatokana na ukatili wa majumbani. Mara nyingi ni wanawake wanaokuja kuomba takaka bila kujali msimamo wa mwanaume.

Vilevile tumepokea pia maombi ya wanaume wanaokuja kuomba kutaliki wake zao baada ya kufikia uamuzi wakutokutaka kuishi nao tena.”

Bi Theopista Mlela (siyo jina lake halisi) – Kijiji cha Ng’ang’ange; ukatili wa majumbani umepungua kwa kweli, wanawake wamekuwa na uelewa zaidi, wanaweza kuomba msaada au talaka.

Mwanaume hawezi kumpiga mke hadharani, akijaribu kufanya hivyo wanawake wote wataungana na kumchangia.”.

Wakijibu kuhusu wanaume kuwapiga wake zao au mwanamke mwingine yeyote hadharani, kikundi cha wanawake kilishangaa sana “…hiyo haiwezekani labda kama anataka kuuwawa,” alieleza Bi Faida Mgonga kutoka kijiji cha Ng’ang’ange.

Katika majadiliano na vikundi mbalimbali vya wanawake, ilionekana wazi kwamba wale wanawake wenye uwezo wakutoa maamuzi kuhusu mali wana uwezo wa kueleza mawazo yao kwa uhuru, kuamua kuhusu suala la kujamiiana, afya ya uzazi, na idadi ya watoto wanayoitaka, na vilevile wana nafasi ndogo ya kukumbana na ukatili wa kijinsia ukilinganisha na wanawake wengine.

Wanawake waliopo katika kitongoji cha Shamba la Saba walieleza kuwa hawawezi kutoa maamuzi kuhusu lini na kwa namna gani wanaweza kujamiiana na wenza wao.

Walisema kuwa kwa mujibu wa mila yao, mke hana maamuzi juu ya wakati na namna gani atafanya tendo la ndoa na mume wake.

Mwanaume ataamua ni wakati gani na namna gani, jukumu la mwanamke ni kufuata maamuzi ya mume. Hata hivyo, tofauti na Shamba la Saba katika sula hilo hilo , wanawake wa Ng’ang’ange walikuwa na haya ya kusema;

Bi Jane (siyo jina lake halisi) mama wa makamu mwenye umri wa miaka 60 alisema, “Mimi ndiye ninayeamua kuhusu wakati gani na namna gani nitafanya tendo la ndoa na mume wangu.

Na kama mume wangu akiamua kulazimisha atajutia kitendo hicho.

Ni mimi pekee ninayelewa mwili wangu. Nina fahamu ni wakati gani niko tayari, au nimechoka, au sijisikii kufanya. Huu ni mwili wangu na ni mimi pekee ninayejua ukoje”

Wanawake katika kijiji cha Itundunu nao hawakua na mtizamo tofauti na wenzao wa Ng’ang’ange, “Ninafahamu mwili wangu unahitaji nini na ndio maana, kwa kweli, nitapata shida kuwa na mwanaume mwenye visingizio visivyoisha.

Najua hana muda na mimi tena, ama niombe talaka au nitafute namna ya kukabiliana na hali, lakini lazima na mimi niwepo katika mpango mzima na siyo yeye pekee.”.

Majadiliano haya yanaonesha uhusianao wa karibu kati ya utoaji maamuzi kwa wanawake, umiliki wa mali, na umasikini, ukatili wa kijinsia na afya ya uzazi.

Uwezo wa mwanamke kutoa maamuzi unapokua mdogo uwezekano wake kuingia katika dimbwi la umasikini na kunyanyaswa ni mkubwa na vilevile kwa upande mwingine kama uwezo wake wa kutoa maamuzi ni mkubwa basi uwezekano wa kujikwamua ni mkubwa.

Mila na dini navyo vimechangia kwa kiasi kikubwa, katika mazingira mengine dini ilitumika kama dhana ya kuwapa wanawake nguvu na katika mazingira mengine ilitumika kama dhana ya kuwakandamiza wanawake na watoto wa kike.

## Vikundi vya Wanawake:Nguvu ya Umoja na Mshikamano

Programu ya AYP ilishirikiana na PAICODEO kuandaa na kutoa mafunzo kwa washiriki 100 wanaowakilisha vikundi vya wanawake wa jamii za kifugaji katika mikoa ya Morogoro na Manyara.

Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo wanawake katika stadi na maarifa katika maeneo waliyobainisha mwanzoni mwa utekelezaji wa programu.

Vikundi vya wanawake vilibainisha mahitaji katika stadi na maarifa ya ujasiriamali, haki za wanawake zinazohusiana ardhi na utatuzi wa migogoro, na mabadiliko ya tabianchi.

Baada ya mafunzo wanawake waliunda vikundi vya wanachama 25 kwa kila kikundi na vyote tayari vilikuwa vimekwishaandaa wazo la biashara.

Baadhi ya wanawake waliweza kutoa mafunzo kwa wanawake wenzao katika vijiji vyao na wanawake hao nao walibuni mawazo yao ya kibiashara au shughuli za kiuchumi ili kujiongezea kipato.

Kuna zaidi ya Vikundi 20 vya wanawake kutoka Manyara na Kilosa, na Mvomero. Jedwali hili linaonesha baadhi tu ya vikundi hivi na biashara zao.

| **Jina la Kikundi** | **Kijiji** | **Shughuli ya Kiuchumi** | **Shughuli ya Kiuchumi Kipato kilichopatikana** | **Kipato kilichopatikana Maelezo/Mipango ya Baadaye** |
|---|---|---|---|---|
| UMAZA (wanachama 25) | Zambia | Kilimo cha Alizeti | 4,000,000 | Kukuza shughuli za kiuchumi mbali na kilimo, ufugaji kuku |
| Baraka (wanachama 25) | Loolera | Ushonaji shanga/ Utengenezaji wa nguo za “Kimaasai (Orkaraha) Kilimo Vikundi vya Kuweka na Kukopa | 380,000 (kiwango cha mchango kwa mwanachama kwa wiki ni 5,000) | |
| Enyora (wanachama 26) | Kilimo na Ufugaji | Ng’ombe wawili | | Hakuna mavuno kutokana na hali ya hewa kubadilika. Wanamipango ya kununua mbuzi |
| Naisula (wanachama 20) | Sokoine | Ufugaji kuku | Alipata kuku 100 | Walipoteza kila kitu wakati wa mchakato wa kuondoshwa ikiwa ni pamoja na kuku ambazo zilikuwa ni mtaji wao. |
| Nawang’ani (wanachama 22) | Sokoine | Sokoine Ufugaji kuku Ufugaji wa mifugo | Kuku 30 Ng’ombe 1 na Mbuzi 6 | Wanauza maziwa ya ngo’mbe na mbuzi kwa ajili kujipatia kipato. |



Majadiliano na wanawake hawa yalionesha wazi kuwa wana mipango mikubwa na wanataka kuinua hali ya maisha yao na ya familia zao. Hata hivyo walielewa kuwa haya yatowezekana kama hawatofanya kazi kwa kushirikiana kwa pamoja.

Kwa mfano; katika mila ya kimasai, wanawake kumiliki ng'ombe au mali itawezekana kwa urahisi zaidi kwa kupitia vikundi vya hiari kuliko kwa mtu mmoja mmoja. Katika vikundi wanakua na uhuru na wanaondokana na kulazimika kusubiri ruhusa ya waume zao; wanaweza kununua ng'ombe, kutengeneza shanga, kulima na kufanya biashara ndogo ndogo.

Biashara ya vikundi huwawezesha wanawake kujipatia mahitaji na kutimiza majukumu kama vile kusomesha watoto, gharama za matibabu, na dharura nyingine ndogo ndogo bila kumtegemea waume au ndugu wengine wa kiume kila wakati.

Wanawake wengi tuliozungumza nao, mbali na kutegemea uuzaji wa maziwa na kilimo ili kuendesha maisha yao, vilevile walikuwa wakikodisha mashamba (kwa pamoja chini ya vikundi) kwa ajili ya kilimo cha biashara (kwa sababu wengi wao wasingeweza kumiliki ardhi peke yao), ufugaji kuku na biashara nyingine za mifugo kama chanzo cha kujipatia kipato.

Wanawake wengine walitengeneza bidhaa za shanga na nguo za kimasai na urembo mwingine mbalimbali ili kujipatia kipato. Wanawake hawa wote walikuwa na changamoto zinazofanana, lakini kubwa zaidi, ilikuwa ni upatakanaji wa masoko na maji.

Mtaji: ili kukabiliana na changamoto ya kupata mitaji kwa ajili ya biashara zao, wanavikundi walikubaliana kutoa michango kwa wiki au mwezi kulingana na taratibu za kikundi.

Pesa iliyopatikana ilitumika ama kukodi shamba la kikundi (kwa ajili ya wanakikundi wote) au kununua ng'ombe, mbuzi, kuku, wa biashara.

Wengi wa wanavikundi hawa, akiba yao ilikuwa ni kati ya shilingi 500,000 hadi 3 milioni kulingana na lini kikundi kilianzishwa au mchango kiasi gani unachangishwa kwa wanachama kwa wiki au mwezi.

Pamoja na kwamba kiasi cha akiba kilikuwa kiko chini, wanawake hawa wana matumaini kuwa kadri muda unavyosonga mbele, akiba itaongezeka na uwekezaji wao wa pamoja utainua hali zao za maisha.

Changamoto kubwa inayokabili shughuli zao za kilimo za wanawake hawa ni mabadiliko ya tabiachi na tofauti kubwa kati ya misimu. Kwa mfano, wanawake wengi walikodi mashamba yenye ukubwa tofauti tofauti kulingana na akiba yao, na baadhi hadi ekari 5, lakini kutokana na ukame hawakuambulia chochote katika mavuno.

Baadhi ya vikundi, kama vile vya kijiji

cha Sokoine, viliondoshwa kutoka katika makazi yao na hivyo vilipoteza kila kitu na hivyo kujikuta vikitumia akiba zao kuanza maisha mapya.

Matukio haya yanaonesha ni kwa kiasi gani mitaji na uwekezaji wao sio endelevu. Sehemu kubwa ya akiba yao ilitumika kugharamia mahitaji ya msingi na dharura badala ya shughuli za kiuchumi.

Masoko: Suala la upatikanaji wa masoko ni moja ya changamoto kubwa kwa wanawake tulioongea nao. Kwa mfano wanawake wafugaji soko lao kubwa ni ndani ya jamii na hii husababisha biashara zao zisikue kulingana na matarajio yao.

Baadhi ya makundi haya walitamani na kuomba msaada wa kuunganishwa na masoko, majukwaa na fursa nyingine zozote za kimasoko ambazo zitasaidia kukuza biashara zao.

Uhaba wa Maji kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi: Uhaba wa maji kutokana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi kama vile ukame umewafanya wanawake kuwa na umaskini unaotokana na kutumia muda mwingi zaidi katika kuchotelea maji visimani.

Wengi wa wanawake hawa walisema wanajikuta hawana muda wa kutosha kwa ajili ya shughuli za kiuchumi. Kama ilivyotajwa hapo juu, kiasi kidogo cha mvua na uhaba wa maji ya umwagiliaji unasababisha mavuno kuwa madogo.

Kwa wanavikundi tuliozungumza nao, wengi wao wamekodi mashamba na kupanda maharage, mahindi, alizeti lakini walipata mavuno machache.

Walitaja vilevile changamoto ya upatikanaji wa taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kwamba pale ambapo taarifa za utabiri wa hali ya hewa za jadi na zile za shirika la utabiri wa hali ya hewa tanzania zilipopatikana nazo hazikuwa za uhakika.

Mabadiliko ya Tabianchi: Utabiri wa Hali ya Hewa wa Jadi

Mabadiliko ya tabianchi ni kati ya tishio kubwa kwa jamii nchini Tanzania hususan jamii zilizoko pembezoni na zinazoishi katika mazingira magumu kama vile jamii za kifugaji na wakulima na hususan wanawake. Tathmini ilifanyika chini ya propramu ya AYP kwa lengo la kuelewa zaidi mbinu zinazotumika na jamii ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Utafiti ulijikita zaidi katika suala la upatikanaji wa taarifa za utabiri wa hali ya hewa hususani katika mfumo wa jadi. Jedwali lifuatalo litaonesha mbinu za jadi za utabiri wa hali ya hewa.

Taarifa zilizokusanywa kuhusu mbinu hizi zitasaidia kuona ni namna gani tunaweza kuunganisha ujuzi wa jadi na ule wa kisayansi ili kupata taarifa za utabiri wa hali ya hewa na hata kujiandaa na athari za mabadiliko ya tabia nchi.



## Viashiria vya Utabiri wa Hali ya Hewa katika jamii ya Kimaasai

| KIASHIRIA | MAELEZO |
|---|---|
| Mwanzo wa msimu wa mvua | |
| Nyota | Kuna nyota 8 zijulikanazo kama ngakwa, lakini nyota zinazotajwa zaidi ni 6 na kadri zinavyokaribiana uwezekano wa mvua kunyesha unakua mkubwa. Kileken (kimondo); ikipita kutoka mashariki kwenda magharibi humaanisha kuwa msimu wa mvua umeanza. |
| Jua na Mwezi | Wakati jua na au/mwezi ukitengeneza mduara (boma) wakati wa msimu wa ukame |
| Utumbo mdogo wa mbuzi | Mbuzi akichinjwa, sehemu ya utumbo mdogo unaokua na maji maji kama mapovu humaanisha msimu wa mvua unakuja |
| Mbuzi dume | Mbuzi dume hupiga kilelee sana usiku |
| Ng'ombe | Ng'ombe wanapokataa kutoka kwenye boma |
| Kichuguu | Ubichi katika kichuguu |
| Miti: Oltepesi (Migunga), Oiti (kikwata), Orng'aroji and Ormame | Miti hii kupata maua |
| Joto | Joto kali |
| Ndege aina ya Ormunguk | Sauti kali inamaanisha mwanzo wa msimu. |
| Mawingu | Mawingu yanaonekana kama michoro ya pundamlia |
| End of rain season | |
| Ukungu | Kinyesi cha ng'ombe chenye Ukungu kutoka midomoni mwa watu wakati wa asubuhi |
| Jua na Mwezi | Mduara unazunguka juan na au/mwezi |
| Mbuni | Akipiga kele usiku kama ile ya simba |
| Fisi | Akitoa kelele ya muda mrefu na ya sauti kali |

## Ishara za utabiri wa hali ya hewa katika jamii ya Wanguu

| | |
|---|---|
| Mwanzo wa msimu wa mvua | |
| Mawingu | Mawingu (kwa kawaida mawingu mawili madogo) ukiwa ni upande wa kaskazini humaanisha mvua (ya wastani) hivyo ni kuanza kupanda. |
| Vipepeo (makunguza) | Vipepeo wa mwezi Aprili (makunguza) wakipaa magharibi kwenda mashariki maana yake kutakuwepo na mafuriko huko vinapoelekea |
| Nyota (kilimila) | Nyota (kilimila) kukutana kwa pamoja mwezi desemba, jua linakua juu |
| Miti (miombo na miembe) | Miembe kupata maua<br>Miombo kupata maua |
| Mwisho wa msimu wa mvua | |
| Mawingu | Mawingu mawili yakionekano na wingu moja likiwa kubwa humaanisha kutakuwa na mwezi wenye ukame. |

## Ishara za utabiri wa hali ya hewa katika jamii ya Wasandawe

| ISHARA | MAELEZO |
|---|---|
| **Mwanzo wa msimu wa mvua** | |
| Chura mweupe wa nchi kavu | Kelele kali ya chura mdogo mweupe anayekua katika paa la nyumba nya tembe zilizoezekwa kwa matope humaanisha kutanyesha usiku kucha. |
| Sisimizi (Th'suu) | Wakionekana humaanisha ni mwanzo wa msimu wa mvua |
| Jua | |
| Miti (Arange) | Mbegu zake zikikomaa ni kiashiria kuwa kutanyesha |
| Ndege | Wakati ndege aina ya "Tooli" akipiga kelele kali humaanisha lazima kunyeshe siku tatu. "Dudumizi", akipiga kelele kali humaanisha lazima kunyeshe, siku hizi anaweza kupiga kelele na kunyesha. |
| Kichuguu | Ubichi juu ya kichuguu maana ni mwanzo wa msimu wa mvua |
| **Mwisho wa msimu wa mvua** | |
| Miti (Arange) | Humaanisha ni mwisho wa msimu wa mvua |

## Namna wanavyotumia utabiri wa hali ya hewa wa jadi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi:

Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, wanajamii wanasema, wakati wa msimu wa ukame au wakiona ishara za kuwapo kwa msimu wa ukame wanatenganisha mbuzi dume na mbuzi jike ili kuhakikisha hawapandani. Kutokana na kwamba mbuzi hawana uwezo wa kutembea masafa marefu kutafua malisho na maji tofauti ilivyo kwa ng'ombe.

Wanajamii inabidi watafute maeneo ya malisho ya karibu ambako mbuzi watapata malisho na maji katika kipindi chote cha ukame. Taarifa kuhusu uwezekano wa kutokea kwa msimu wa ukame na njaa hutolewa katika mkutano baina ya wanakijiji na uongozi wa kijiji.

Mwanajamii mmoja alisema kuwa mabadiliko ya tabianchi, yanaathiri siyo tu maisha yao kijamii lakini kiuchumi pia kwani inakua vigumu kuwa na mbuzi wengi zaidi, na mara nyingine hata hao wachache waliopo nao hufa kutokana na kukosa maji.

Waliongeza kusema kuwa kwa wale wafugaji wanaotegemea ng'ombe kama chanzo cha kipato basi madhara ni makubwa sana kiasi kwamba ni vigumu hata kukadiria.

Mipango ya umwagiliaji ili kuwezesha shughuli za kilimo:

Mpango wa umwagiliaji ulianzishwa kwa lengo la kusaidia shughuli za kilimo wakati wa msimu wa ukame. Hata hivyo, changamoto inayojitokeza ni kwamba wakati wa vipindi vya mvua kali, miundo mbinu ya umwagiliaji huaribiwa na mara nyingi huvunjika na kuwaacha wakulima katika hali ya hatari iwapo msimu wa ukame utafuata. Miundo mbinu ya umwagiliaji iliopo haina uwezo wa kuvuna maji ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji.

Mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Wanajamii hushiriki katika kusafisha na kutunza miundo mbinu ya umwagiliaji. Wakati wa ukame au vipindi vya mvua kidogo wanajamii hushauriwa kupanda mazao yanayostahimili ukame.

Kwakutumia taarifa za utabiri wa hali ya hewa zinazotokana na mifumo yote miwili ya jadi na ya kisayansi husaidia wanajamii kujiandaa vizuri zaidi. Taarifa hizi ni muhimu zaidi leo hii kutokana na ukweli kwamba mabadiliko ya tabianchi yamekuwa ni dhahiri. Kuna mapokezi ya ujuzi na maarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, cha wazee kwenda kwa vijana.

Mwanajamii mmoja alisema," Mabadiliko ya tabianchi ni mipango ya mungu, hakuna unaloweza kufanya lakini kuna uwezekano wa kujiandaa kuhusu namna ya kukabiliana na mabadiliko yenyewe kulingana na hali itakavyokua baada ya msimu wa mvua nyingi au ukame mrefu".

Ubunifu na uzuri uliopo katika tamaduni Programu ya AYP na washirika wake walilenga kujifunza kuhusu namna ambavyo maisha ya wanaume na wanawake yanavyoathiriwa kwa namna moja au nyingine na mila na desturi.

Shuhuda zifuatazo kutoka katika jamii za Wamaasai na Wahehe, kati ya makabila mengine mengi, zinaelezea namna ambavyo mila na desturi zao zinavyotafsiri mambo yafuatayo:

mgawanyo wa majukumu katika jamii, umiliki wa mali, na masuala mengine ya kitamaduni yaliyomuhimu katika jamii hizi.

**Mgawanyo wa Majukumu**

**Wamaasai**

Katika kijiji cha Loornderkes; mgawanyo wa majukumu kati ya wanaume na wanawake umewekwa bayana. Wanaume wanajukumu la kununua chakula katika kaya, kuchunga ng'ombe na kulinda jamii. Wanawake wana jukumu la kazi za nyumbani, kulea watoto na wazee, kuangalia ndama katika maeneo ya nyumbani. Akifafanua kuhusu majukumu ya wanaume na wanawake, Bi Sabina Daniel alisema; "Wanaume wao hununua mahindi tu basi, alafu wanawake wanahakikisha kuwa mahindi hayo yametwangwa na kutafuta vitu



vingine kwa ajili ya kula na ugali, hayo ni makumu yetu wanawake".

Bi Paulina Lazaro mwanakikundi mwingine alisema, "Ukiangalia mgawanyo wa majukumu katika mila yetu, wanawake wanafanya kazi nyingi zaidi kuliko wanaume, wanaume huleta vitu vya kuanzia tu alafu sisi ndio tunahangaika kukamilisha na kuhakikisha familia inakula". (Picha ya Wanawake wakijadiliana katika vikundi)

**Wahehe**

Ndugu Mistedy Kipingi kiongozi wa kimila wa kihehe kutoka kijiji cha Ng'ang'ange anasimulia kuhusu majukumu ya ya wanaume na wanawake katika mila zao; "Katika mila yetu, mwanaume hujenga nyumba na mara baada ya nyumba kujengwa inakuwa ya mke wake na watoto na mwanamke hushughulika na kazi za nyumbani, kulea watoto na wazee nyumbani."

Akiongeza alichoeleza kiongozi huyo wa mila, Bi Kihwele alisema; "tukija kwenye upande wa kilimo, wanaume huandaa mashamba na wote tunalima."

**Umiliki wa Mali**

**Wamaasai**

Mtoto akizaliwa bila kujali kama ni wa kike au wakiume, atapewa ng'ombe, mbuzi, au kondoo. Mtoto wa kike akiolewa, anaweza kuondoka na nusu ya ng'ombe kwa sababu inategemewa kuwa nyumbani kwa mume atapewa ng'ombe wa kwake.

Lakini kwa upande wa umiliki, wanaume na wanawake walikuwa na mitazamo tofauti. Wanawake wengi waliona kuwa wao walitunza tu ng'ombe lakini siyo kuwamiliki au kutoa maamuzi yeyote juu yake, lakini wanaume kwao waliona kuwa hiyo ni umiliki (Laigwanan-tafuta jina hili)

**Wahehe**

Kimila, wahehe ni jamii ambayo

mwanaume anaweza kuoa mke mmoja na zaidi,lakini anayetambulika ni mke mkubwa tu huku mke au wake wengine wakichukuliwa rafiki wa mume.

Mume akioa mke wa pili, inachukuliwa kwamba anatumia mali kutoka katika ndoa yake ya kwanza kwa ajili ya kulipa mahari.

Hivyo basi inachukuliwa kuwa mke wa kwanza naye ni kama vile ameoa hawa wake wengine wapya na hivyo watahesabika ni wake zake pia. Kama mume akifariki, watoto kutoka kwa mke wa pili watatambulishwa rasmi kwa mke wa kwanza wakati wa msiba. Wake wengine au wanafamilia hawawezi kudai mali kutoka kwa mke wa kwanza, kila kitu ni mali yake na watoto.

Kama mke ndiye aliyefariki, mume anaweza kuoa mke mwingine lakini hatoruhusiwa kumleta mke wa pili katika nyumba ya mke wa kwanza isipokuwa tu kama yule mke wa kwanza hakuwa na watoto.Hali hii hupunguza misuguano mingi katika familia na kuepusha migogoro isiyo ya lazima.







## Ubunifu katika vazi la Kimaasai Orkaraha

Orkaraha (nguo) ni vazi lenye matumizi mbali mbali ikiwemo kutumika katika sherehe, kulinda joto la mwili kulingana na hali ya hewa, na vilevile hutumika kama begi la kubebea mzigo, na hata kujitanda kwa wanawake. Akina mama wa Kimasai pia hulivaa vazi hilo kulingana na hali ya hewa, kama ikiwa baridi laweza tumika kama mtandio, kufunika kichwa na kadhalika. Ikiwa wakati wa joto uvaaji wa Orkaraha hubadilika. Aidha, jamii hii inaamini kuwa kwakumiliki vipande vichache tu vya nguo kutasaidia kupunguza kasi ya mabadiliko ya tabianchi, kwani kuwa na nguo nyingi husababisha kuwepo na viwanda vingi zaidi na hivyo kuharibu zaidi hali ya hewa.


























YALE
FORESTRY

CARE International Tanzania
Mtaa wa Ruhinde , Nyumba Na. 195 B | P.O. Box 10242 - Dar es Salaam, Tanzania
Simu: : +255 22 2668061 | fax: +255 22 2666944
Tovuti: care-tanzania.org
Hakimiliki © 2019 Cooperative for Assistance and Relief Everywhere, Inc. (CARE)
Picha zote © 2019 Mwanzo Millinga/CARE